BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Ishirini na Tano – Tarehe 13 Juni, 2023
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

MASWALI:

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

237. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Katika Kware iliyoko Makaani, katika kijiji cha Vitongoji Wilaya ya Chake Chake Mkoa wa Kusini Pemba, kumekuwa na ongezeko kubwa la mashine za kusaga kokoto (crushers). Maeneo hayo yanatumiwa na wananchi wanyonge na walipa kodi wa nchi hii kwa ajili ya kilimo na mifugo yao na hivyo huondoshwa bila ya kulipwa chochote katika ardhi hizo ambazo zingewasaidia kusukuma maisha yao kwa kipindi kirefu.

(a) Je, Serikali kwa kiasi gani inalitambua jambo hilo.

(b) Je, Serikali itawasaidia vipi wanyonge hao kuepukana na unyanyasaji huo unaofanywa na matajiri.

(c) Je, vitendo hivyo vya matajiri dhidi ya wanyonge katika maeneo hayo, vinapingana vipi na malengo ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964.

Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

200. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Migogoro mingi ya ardhi katika jimbo la Pandani inawahusu wananchi wanyonge wa kawaida na masheha au manaibu wao, na kwa kiasi kikubwa kuna malalamiko ya kupuuzwa kwa wananchi hao ukilinganisha na masheha au manaibu wao.

(a) Je, Serikali inaufahamu mgogoro wa ardhi kati ya Sheha wa shehia ya Kiungoni na mwananchi wa kawaida katika kijiji cha Kimango na lini mgogoro huo utapatiwa ufumbuzi.

(b) Je, Serikali inaufahamu mgogoro wa ardhi kati ya Serikali ya Mkoa na mwananchi wa kawaida katika kijiji cha Machengwe ambapo ardhi ya umiliki binafsi imechanganywa na ardhi ya eka na kumilikishwa mtu mwengine na lini mgogoro huo utapatiwa ufumbuzi.

(c) Kwa kuwa utatuzi wa migogoro mingi umekuwa ukiwanyima haki wananchi wanyonge, je, ni upi mpango wa Serikali wa kumaliza migorogo kistaarabu hasa ya umiliki wa ardhi katika maeneo ya uwekezaji kwenye migogoro kati ya Serikali na wananchi.

Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

172. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

(a) Tathmini ikoje juu ya upatikanaji wa soko la mazao ya viungo kimataifa.

(b) Ni taasisi zipi ambazo zinajikita kununua mazao ya viungo na kusafirisha nje ya nchi.

(c) Je, ni upi uwezo wetu wa kuzalisha mazao ya viungo vyenye kumudu soko la kimataifa kwa wazalishaji wetu wa ndani na upi mkakati wa Serikali wa kuwainua wazalishaji wa bidhaa za mazao ya viungo nchini.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

190. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Serikali kwa nia safi kabisa imeanzisha karakana kuu ya magari huko Chumbuni kwa Unguja na Tibirinzi Chake Chake kwa upande wa Pemba.

(a) Je, ni kwa utaratibu upi Serikali inayapeleka magari yake kwa ajili ya matengenezo katika karakana yetu hiyo.

(b) Je, kwa kipindi cha 2020-2023, ni magari mangapi ya Serikali yamepelekwa kwa ajili ya matengenezo na mangapi yalipelekwa kwenye karakana binafsi.

**Wizara ya Afya:**

214. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Ni jambo jema kwamba Serikali imeweka Kitengo cha Viungo Bandia kilichopo katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Hata hivyo, pamoja na ukweli kwamba kitengo hicho kina wataalamu wa viungo bandia, lakini bado hakioneshi kuwa na bajeti yoyote ya kununua malighafi ambayo ndio msingi mkuu wa kazi zao.

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kimetengwa na Serikali na kiasi gani kilipatikana kwa ajili ya matumizi ya Kitengo cha Viungo Bandia kwa kipindi cha 2020-2023.

(b) Je, ni upi utaratibu wa kupata viungo bandia kwa wananchi wa Zanzibar walio Wazanzibari na wasio Wazanzibari wenye mahitaji na ulazima wa kupata viungo hivyo.

(c) Je, ni upi uhusiano wa Kitengo cha Viungo Bandia na Baraza la Watu Wenye Ulemavu Zanzibar na ni kwa nini wahitaji wa viungo bandia hutozwa fedha kupitia vitengo vya nje ya hospitali.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

83. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kumekuwa na tatizo la vyoo katika skuli ya shehia ya Mtangani sekondari na msingi kwa sababu vyoo vilivyokuwepo vimekuwa havifai kutumiwa. Hali hii inawapelekea baadhi ya wanafunzi

kukimbilia kwa majirani kwa ajili ya kutekeleza haja zao, jambo ambalo sio zuri.

(a) Je, Wizara yako inalitambua vipi suala hili.

(b) Je, ni lini tatizo hilo litaondolewa.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

208. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kama zilivyo Serikali za nchi nyingi duniani, Serikali yetu pia imekuwa ikijipanga kupiga vita na kujiweka tayari dhidi ya maradhi nyemelezi. Hata hivyo, mfumo wa maisha, wataalamu tulionao na sehemu za mazoezi zilizopo hazionyeshi kuwa tunaweza kujiepusha na maradhi hayo.

(a) Je, Serikali ina mpango gani maalumu wa kuwazindua watu juu ya maradhi nyemelezi, jinsi ya kujikinga na kuwa na mfumo bora kiafya wa maisha (Healthy Lifestyle).

(b) Je, Serikali inavisaidi vipi vyama vya mazoezi nchi nzima katika kupatikana vifaa na wataalamu wa mazoezi.

(c) Je, kwa nini Serikali haitoi punguzo maalumu la kodi na kutoa bahshishi kwa wawekezaji wa sehemu za mazoezi (Gyms) ili kurahisisha kupatikana maeneo ya kufanyia mazoezi.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

135. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Pamoja na juhudi kubwa za Serikali katika kuwawezesha wananchi wetu hususan vijana kuingia katika sekta ya kilimo, bado juhudi hizo zinaonekana zaidi kinadharia kuliko vitendo.

Je, Wizara inatumia mikakati gani ya kuwashawishi vijana kuingia katika uzalishaji wa sekta ya kilimo kwa vitendo.

224. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Moja kati ya mambo yaliyoitambulisha Zanzibar kimataifa ilikuwa ni kwa uzalishaji wa viungo. Hata hivyo, nguvu ya Serikali ya kuzalisha viungo nchini inapungua siku hadi siku.

(a) Je, Serikali inasimamia vipi utekelezaji wa sera bora ya viungo (Zanzibar Spices Policy).

(b) Je, kwa kiasi gani Serikali inasimamia uimarishwaji wa kilimo cha viungo (spices) ili kufanya viungo viwe zao jipya la kibiashara.

(c) Je, Serikali haioni haja ya kuanzisha na kurasimisha Mkakati wa Uendelezaji Viungo (Zanzibar Spice Development Strategy (ZSDS)).

**<u>Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:</u>**

162. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Ni maeneo gani ya kihistoria ambayo wataalamu wetu wa mambo ya kale wanaojikita na taaluma ya kiakolojia wameweza kuyavumbua kwa miaka ya hivi karibuni na maeneo hayo yana umuhimu gani katika historia ya Zanzibar.

**Zanzibar,**
**13 Juni, 2023.**

**(Raya Issa Msellem)**
**<u>KATIBU WA BARAZA</u>**